# KISWAHILI LUGHA

# DARASA LA SABA

# 2015


**AVAILABLE ONLINE AT:**

Schools Net Kenya Consultancy

**P.O. Box 8076 – 00200 Nairobi, Kenya | Tel: +254202319748**

**E-mail: infosnkenya@gmail.com | www.schoolsnetkenya.com**

# KISWAHILI
# SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Kamilisha methali: Mwenda pole

A. hafiki
B. haanguki
C. hajikwai
D. hafanikiwi

Jibu sahihi ni **C**

**1** A B C D    **11** A B ~~C~~ D    **21** A B C D    **31** A B C D    **41** A B C D

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi **C** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15.** *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Siku hiyo jua ____**1**____ kuchomoza miale ____**2**____ asubuhi na mapema. Upepo mwanana ____**3**____ na kuifanya siku ____**4**____ iwe ya ____**5**____ kwa fani za michezo. Mashindano ya kutembea kasi ____**6**____ yaliyoanza, ____**7**____ na mashindano ya kukimbia ndani ya magunia. Mbio hizo ____**8**____ mno wote waliohudhuria.

**1.** A. ulianza B. ilianza C. lilianza D. lilianzisha

**2.** A. yake B. zake C. wake D. zao

**3.** A. ilivuma B. ulifuma C. ulichomoza D. ulivuma

**4.** A. enyewe B. yenyewe C. yenye D. lenyewe

**5.** A. kipekee B. peke C. pekee D. poa

**6.** A. ndio B. ndipo C. ndiyo D. ndiye

**7.** A. ikafuatwa B. yakafuatiwa C. yakafuatwa D. yakafutana

**8.** A. zilisheherekewa B. ziliwadunisha C. ziliwafedhehesha D. ziliwafurahisha

Taifa ____**9**____ hapa duniani ____**10**____ vijana ____**11**____ katika ujenzi wa taifa. Ni kweli kuwa vijana ____**12**____ nguvu hutupa matumaini ____**13**____ ya nchi ____**14**____ katika siku za usoni. Ni ____**15**____ wetu basi kuwalea kwa maadili mema ya jamii bora.

**9.** A. lolote B. yoyote C. wowote D. lote

**10.** A. hutega B. hutengana C. hutegemea D. hutengea

**11.** A. vyake B. wake C. yake D. zake

**12.** A. wenyewe B. vyenye C. lenye D. wenye

**13.** A. kubwa B. ndogo C. madogo D. makubwa

**14.** A. thabiti B. dhabiti C. hafifu D. nzuri

**15.** A. lengo B. jukumu C. wajibu D. nia

*Kati ya maswali* **16 - 30,** *chagua jibu sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16.** Ukiambiwa kwaheri, utajibu
A. asante
B. inshallah
C. tutaonana tena
D. ya kuonana

**17.** Kipofu __________ alijikata kidole.
A. chenyewe
B. mwenye
C. mwenyewe
D. yenyewe

**18.** Kamilisha methali: Jungu kuu
A. halikosi ukoko
B. lapika vizuri
C. hupika vyema
D. halikosi ugali

**19.** Utakapofika; tafadhali tupigie simu. 'po' imetumika kuonyesha
A. matarajio
B. wakati
C. mahali
D. sababu

**20.** Ndugu wa kike wa baba ni
A. shangazi
B. binamu
C. mpwa
D. wifi

**21.** Chagua sentensi iliyo sawa kisarufi
A. Mahali pale kwenyewe ndipo mmefagiliwa
B. Mahali mle mwenyewe ndipo pamefagiliwa
C. Mahali kule kwenyewe ndipo kumefagiliwa
D. Mahali pale penyewe ndipo pamefagiliwa

**22.** Ni salamu ipi ambayo si ya wakati wowote?
A. Sabalkheri
B. Hamjambo
C. Waambaje
D. Cheichei

**23.** Mwalimu <u>mgeni</u> ameripoti leo shuleni. Neno lililopigiwa mstari ni
A. kiashiria
B. kivumishi
C. kitenzi
D. kielezi

**24.** Walipokuwa <u>wakisoma</u>, chakula kililetwa mezani 'ki' imetumika kuonyesha
A. masharti
B. wakati
C. udogo
D. kielezi

**25.** Jua ni juvya kama vile ogopa ni
A. ogopana
B. ogovya
C. ogofya
D. ogopesha

**26.** Chagua sentensi iliyotumia nomino ya makundi.
A. Uzalendo ni kitu adhimu
B. Niazime shilingi kumi nitumie
C. Batamzinga alichinjwa jana
D. Genge la wezi lilivamia jana

**27.** Wingi wa: Uyoga wake umeliwa na seremala
A. Uyoga wao umeliwa na maseremala
B. Yoga zao zimeliwa na maseremala
C. Uyoga wao umeliwa na seremala
D. Mayoga yao yameliwa na maseremala

**28.** Chagua maneno yaliyo katika ngeli ya Li-Ya
A. jino, shauri, kichwa, uta
B. gari, umbo, pazia, jiko
C. upishi, blanketi, ubua, uele
D. ubavu, udevu, uzi, uso

**29.** Chagua kundi lenye viunganishi pekee
A. Lo! Alas! Aah! Ewaa!
B. Juu ya, baada ya, chini ya
C. Ila, iwapo, wala, au
D. Cheza, lia, oga, lala

**30.** Fundi wa kutengeneza vitu vya mapambo kwa dhahabu ni
A. seremala
B. sogora
C. sonara
D. mhunzi

*Soma habari hii kisha ujibu maswali* **31 – 40**

Ulimwengu wa sasa umeshuhudia janga jingine la maradhi ya Ebola. Hata kama gonjwa hili halijakita mizizi kama ndugu yake UKIMWI, linatishia maisha ya binadamu hata kabla ya siku ya kiyama kufika. Kwa vile hatujui mengi kuhusu zimwi hili, ebu tutaje machache kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

Gonjwa hili liligunduliwa nchini Kenya mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1984. Tangu wakati huo, mauti yamevuma kupitia kwalo hadi mapengo yaliyoachwa hayawezi kamwe kuzibika.

Jamani! Ugonjwa wa UKIMWI una madhara mengi na unaweza kuambukizwa mtu yeyote yule kupitia njia mbalimbali. Mojawapo ni kutumia sindano, wembe, visu na vifaa vyovyote vile vyenye ncha kali. Vifaa hivi vikikukata huweza kukuletea madhara hayo. Njia hii sanasana hutumiwa na baadhi ya vijana wanaotumia dawa za kulevya kama kokeini kwa kujidunga sindano moja kwa moja ili kutekeleza wajibu wao waliokusudia.

Aidha gonjwa hili linaweza kuambukizwa malaika kupitia maziwa ya mama zao wale tayari wana virusi hivi. Hi ni wazi kuwa mama anaponyonyesha mtoto bila kujua kama ameathirika, hujikuta amesambaza ugonjwa huu kwa kiumbe hiki kisichojua mbele wala nyuma.

Kule hospitalini, matabibu wanaweza kumpa damu mgonjwa mwingine bila damu yake kuchunguzwa ipasavyo. Ni sharti waichunguze damu yoyote hata kama mgonjwa yule yu katika hali mahututi ina paswa asubiri kwa sababu subira huvuta heri.

Njia nyingine inayoeneza ugonjwa huu wa UKIMWI ni kupitia ngono-ashakuna si matusi. Kitabu kitakatifu kinasema mili yetu ni hekalu ya roho mtakatifu. Kwa hivyo hatuna budi kujiheshimu. Wahenga hawakukosea waliposema mchovya asali hachovi mara moja. Aidha kinga ni bora kuliko tiba.

Ni jukumu letu basi kama viongozi, wazazi, walimu na wanafunzi wenzangu kujihadhari kabla ya athari ili jamii yetu ikue kwa njia mwafaka na kuendelea kujenga nchi yetu daima dawamu.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, mwandishi anasema
A. Ebola ndilo janga la pekee ulimwenguni
B. ulimwengu haujashuhudia majanga mengine
C. hili ndilo janga la kwanza humu nchini
D. kulikuwa na majanga mengine hapo awali

**32.** Mwandishi hajatueleza mengi kuhusu Ebola kwa sababu
A. siku ya kiyama haijafika
B. ni ugonjwa ambao unatisha sana
C. hafahamu mengi kuhusu ugonjwa huu
D. anangoja likite mizizi kama UKIMWI

**33.** Ni miongo mingapi imepita tangu maradhi ya UKIMWI yagunduliwe humu nchini?
A. 3
B. 30
C. 4
D. 31

**34.** Ni kifaa kipi kati ya hivi hakina ncha kali?
A. Sindano
B. Wembe
C. Mkuki
D. Mfuko

**35.** Vijana wanatumia dawa za kulevya ili kutekeleza wajibu wao. Hii ina maana kuwa
A. vijana wote ni sharti wazitumie
B. dawa hizi hutawala mawazo yao
C. dawa hizi zinapendeza zaidi kiafya
D. dawa hizi zinawafaa vijana wote

**36.** Mwandishi ametumia neno malaika kumaanisha
A. kiumbe kutoka mbinguni
B. watoto wandogo sana
C. nywele zipatikanazo mwilini
D. watoto bado hawajazaliwa

**37.** Malipo yatolewayo kwa kumtoa mtu damu huitwa
A. kiingilio
B. fola
C. arshi
D. ushuru

**38.** Mgonjwa kuwa katika hali mahututi ni sawa na kusema
A. amepona kabisa
B. amepata ashikeli
C. ameaga dunia
D. yu mgonjwa sana

**39.** Ni methali ipi kati ya hizi si ya kutahadharisha
A. mchovya asali hachovi mara moja
B. kinga ni bora kuliko tiba
C. subira huvuta heri
D. jungu kuu halikosi ukoko

**40.** Kichwa kinachofaa habari hii ni
A. Jihadhari kabla ya athari
B. Magonjwa hospitalini
C. Magonjwa ya Ebola na UKIMWI
D. Jukumu la viongozi

*Soma taarifa hii kisha ujibu maswali* **41 – 50**

Kenya kama nchi nyingine inasemekana kuwa idadi ya ngoma zinazorekodiwa inaongezeka maradufu kila uchao. Sekta hii ya muziki inaendelea kuimarika kiasi kwamba taifa letu linaendelea kutambulikana kwa muziki bora kama vile Angola, Afrika Kusini na Kongo.

Hata hivyo baadhi ya wanamuziki chipukizi wamesikika wakilalamika kuwa yamkini nia yao ya kuiweka Kenya katika ramani ya mataifa yanayosifika kimuziki ikasalia kuwa ndoto iwapo kazi yao haitachukuliwa kwa umuhimu mkubwa na serikali.

Kwa mfano inasemekana ufisadi umechukua mkondo mpya kwa sababu baadhi ya wacheza muziki redioni au katika runinga wanatumia njia za mkato kuuza miziki yao. Hivyo basi hawapati faida ya jasho lao.

Mmoja wa wasanii wa muziki amesema kuwa wanamuziki wanadhulumiwa na hawapewi haki yao. Mara nyingi wanaocheza muziki hawakwambii waziwazi utoe pesa bali wanakuachia wewe kuelewa lugha na matendo kutaka kitu kidogo.

Kando na malalamiko haya, serikali inawahimiza wanamuziki wasiwe na pupa ya kurekodi kazi ambayo haijakuwa tayari ili iwe bora na kupendeza zaidi. Kuna mipango mahususi inayopangwa kuwapeleka baadhi ya wanamuziki ufaransa na mataifa kadha ya Africa ili kujielimisha zaidi jinsi wanavyoweza kujiendeleza kimuziki. Mipango hii ikikamilika, kutakuwa na mwamko mpya na kelele hizo zote zitaweza kupungua.

**41.** Idadi ya ngoma zinazorekodiwa inaongezeka maradufu... inamaanisha
A. inaongezeka mara mbili
B. inapungua zaidi
C. inaongezeka mara kumi
D. inaongezeka mara moja

**42.** Mataifa yaliyotajwa hutambulikana kwa sababu ya
A. kuwa marafiki wa Kenya
B. ukuaji wa uchumi
C. kuwa na madini mengi
D. uchezaji muziki mzuri

**43.** Katika aya ya pili mwandishi anasema
A. ndoto yao inaendelea vizuri
B. ndoto yao inadidimia mno
C. kuna matumaini kupitia muziki
D. wanafurahia kuwa katika muziki

**44.** 'Kitu kidogo' kinaweza pia kuitwa yote haya ila
A. hongo
B. chai
C. muziki
D. rushwa

**45.** Wanamuziki wanaelekeza malalamiko yao kwa
A. wazazi
B. wateja
C. wananchi
D. serikali

**46.** Wanamuziki chipukizi ni wale
A. wanaoanza kujitokeza kimuziki
B. waliobobea kimuziki sana
C. hawapendi muziki kamwe
D. wanaotaka kuhongwa sana

**47.** Serikali imewaonya wanamuziki wasiwe na pupa kukimbilia kurekodi kwa sababu
A. mataifa mengine hayatawaruhusu
B. haina pesa ya kuwalipia gharama
C. kiwango cha muziki wao ki chini
D. Kenya si nchi ya muziki

**48.** Ni taifa lipi ambalo si la bara la Africa?
A. Angola
B. Kongo
C. Uhabeshi
D. Ufaransa

**49.** Ni hatua gani serikali imechukua kukabiliana na tatizo hili?
A. kuwawekea wanamuziki vikwazo vya muziki
B. mipango ya kuwazuia wanamuziki kuendelea
C. mipango ya kuwapeleka wanamuziki nje kusoma
D. kuwafunga wote ambao wanashiriki hongo

**50.** Kichwa cha habari hii ni
A. Kipawa cha muziki
B. Wanamuziki wetu
C. Mwamko mpya wa wanamuziki
D. Wanamuziki fisadi